



## **CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR**

### **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA KIGODA CHA TAALUMA CHA ABEID AMANI KARUME CHA UKOMBOZI NA MAENDELEO YA AFRIKA**

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinatangaza nafasi ya kazi ya Mwenyekiti wa Kigoda cha Taaluma cha Abeid Amani Karume cha Ukombozi na Maendeleo ya Afrika. Dhamana ya nafasi hii itanza tarehe 1 Juni, 2024.

Kigoda hiki cha Ukombozi na Maendeleo ya Afrika kimeanzishwa na SUZA kwa heshima ya kumuenzi Mwanamapinduzi, Hayati Abeid Amani Karume kutokana na mchango wake katika ukombozi na maendeleo ya Zanzibar, Tanzania na Afrika. Hayati Karume alikuwa ni Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SUZA inakaribisha maombi kutoka kwa wanataaluma wabobezi kwenye fani ya taaluma za sayansi ya jamii na insia (humanities). Muombaji wa nafasi hii anatakiwa awe amebobea katika falsafa za Kiafrika, Umajumui wa Kiafrika (*Pan-Africanism*), pia awe na mtandao mkubwa wa kitaifa na kimataifa.

#### **Majukumu**

Mwenyekiti atatarajiwa:

- Kuandaa na kutoa mihadhara, ikiwa ni pamoja na risala ya uzinduzi wa Kigoda ambayo itachapishwa na SUZA.
- Kufanya tafiti na kuanzisha miradi ya kijamii au kitamaduni yenye tija kwa SUZA.
- Kusaidia SUZA kuongeza rasilimali kwa njia za kuhamasisha michango kwa wadau mbalimbali au njia nyinginezo ili kuimarisha uhai wa Kigoda.

#### **Muda wa Utumishi**

Mwombaji atakayefanikiwa atatumikia nafasi ya uenyekiti kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na kutakuwa na uwezekano wa kuongeza utumishi wa nafasi hii kwa muhula mwingine wa kipindi kama hiki.

## **Jinsi ya kuomba**

Waombaji wanapaswa kuwasilisha yafuatayo kwa Katibu wa Timu ya Utafutaji kupitia kwa Makamu Mkuu wa Chuo ([vc@suza.ac.tz](mailto:vc@suza.ac.tz)).

- Barua ya maombi ya nafasi ya Uenyekiti wa Kigoda yenye maelezo ya kujitosheleza.
- Maelezo binafsi (CV).
- Pendekezo la Mpangokazi kwa kipindi cha Uenyekiti (si zaidi ya kurasa 5).
- Barua tatu za Wadhamini zitakazotumwa moja kwa moja kwa Makamu Mkuu wa Chuo ([vc@suza.ac.tz](mailto:vc@suza.ac.tz)).
- Waombaji watakochoaguliwa wataitwa kwa mahojiano ya moja kwa moja.

**Mwisho wa Kupokea Maombi:** Tarehe 3 Mei, 2024.

Waombaji wana jukumu la kuhakikisha kuwa nyaraka zinazohitajika zinakamilika na kuwasilishwa kabla ya tarehe ya mwisho.

Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia: [kigoda.karume@suza.ac.tz](mailto:kigoda.karume@suza.ac.tz)